# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA

Shule ya Sekondari Bumangi,
S.L.P. 208,
**MUSOMA.**

Namba ya Simu:
0754062555/0782974707
0757791556
FAX N0. ………………….

Kumb.Na BMG.SS/BTM/JI/FV/18/01

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………………………………………………

S.L.P. …………………………

……………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI BUMANGI, WILAYA YA BUTIAMA MKOA WA MARA MWAKA 2018**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka **2018** tahasusi ya **PCM,PCB.** Shule ya Sekondari **BUMANGI** ipo umbali wa Kilometa 45 Mashariki mwa mji wa **MUSOMA** Usafiri wa basi kutoka mjini **MUSOMA** unapatikana katika kituo cha mabasi **BWERI**, nauli ni shilingi **3,000/=** pia shule ipo umbali wa km 12 kaskazini mashariki kutoka Butiama mjini,nauli ni shilingi 1,000/=

   Muhula wa masomo unaanza tarehe 02/07/2018, Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 29/06/2018 na Mwisho wa kuripoti ni 08/07/2018

2 **Mambo muhimu ya kuzingatia.**

**2.1 Sare ya shule**

a) Sare ya shule hii ni Surua mbili za bluu bahari na shati nyeupe, pea mbili mikono mifupi.

b) Bukta mbili za bluu na T- shirt 2 za kijani.

c) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vya visigino vifupi jozi mbili.

d) Soksi jozi mbili nyeupe.

e) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa Ngozi.

f) Sweta moja la rangi ya kijivu.

g) Suruari mbili za khaki za kushindia na t- shirti mbili za bluu.

h) Ndoo mbili za lita 20 nyekundu.

i) Raba za michezo aina yoyote na soksi zake.

j) Kidumu cha lita 5 cha maji ya kunywa.

k) Mashuka pea mbili rangi ya kijani, blanketi moja , foronya moja, chandarua moja,

l) Vyombo vya chakula (sahani, bakuri, kijiko na kikombe

m) Godoro futi tatu, inchi nne

n) Ream moja ya karatasi A4.

0) Vitabu vya masomo husika

p) Scientific calculator no. 991.

q) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biology

r) Mifagio ya ndani na nje

s) Jembe lenye mpini kwa wanafunzi wa PCB na fyekeo kwa PCM

t) Madaftari makubwa ya kutosha kulingana na masomo husika.

**Michango**

1. Ada ya Shule kwa mwaka Tshs 70,000/= au Tshs 35,000/= kwa muhula.
2. Malipo mengine
   - i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
   - ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
   - iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
   - iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
   - v. Shilingi 2,000/= nembo ya shule
   - vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza.
   - vii. Shilingi 20,000/= Mitihani mock.
   - viii. Fedha ya tahadhari 5000/= (haitarejeshwa).

**Angalizo:**

Jumla ya ada na michango kwa mwanafunzi ni 178,000/= zilipwe kweny akaunti

**3031200313 NMB**

3. **MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:**
   - i) Wizi
   - ii) Kutohudhuria masomo zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
   - iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
   - iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/wakazi na jamii kwa ujumla.
   - v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
   - vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni na haruhusiwi kunyoa mtindo wa aina yoyote.
   - vii) Kuvaa nguo za kubana.
   - viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
   - ix) Uvutaji wa sigara.
   - x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
   - xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
   - xii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
   - xiii) Kutembelea majumba ya starehe, nyumba za kulala wageni na nyumba za walimu.
   - xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
   - xv) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

4. **Viambatanisho na fomu muhimu**
    a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
    b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo , fujo na makosa ya jinai.
    c) Fomu ya mzazi kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekzo mengine yatakayotolewa na shule.
    d) Picha nne (4) za Wazazi au Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea/kuwasiliana na mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Saini ya Mkuu wa Shule: ..........................................................

Jina la Mkuu wa Shule: KYANGWE L ..........................................................

Mhuri wa Mkuu wa Shule: K.n.y. AFISA ELIMU SEKONDARI HALMASHAURI YA WIL... BUTIAMA ..........................................................

# B UTIAMA DISTRICT COUNCIL
## . REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

PART: A:

DATE .................

TO THE MEDICAL OFFICER.

..............................................

..............................................

- MR/MISS ..........................................................................................

(Name in full)

Please examine the above named as to his/her Physical and mental fitness enrolment as a secondary school student. The examination should include the following categories:

(a) Eye – sight
(b) Hearing
(c) Limbs
(d) Speech
(e) General diseases
(f) Lepresy
(g) Epilepsy
(h) Abdomen
(i) TB.

I. Neuroses
II. Other serious diseases
III. Pregnancy.

PART B:

## MEDICAL CERTIFICATE.

(To be completed by government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that * he/she is physically * Fit and mentally F t for enrolment as a secondary school student.

I. (a) Eye-sight ..........................................................................................
(b). Hearing ..........................................................................................
(c). Limbs ..........................................................................................
(d). Speech ..........................................................................................
(e). General diseases ..........................................................................................
(f). Lepresy ..........................................................................................
(g). Epilepsy ..........................................................................................
(h). Abdomen ..........................................................................................
(i). TB ..........................................................................................

I. Neuroses ..........................................................................................
II. Other serious diseases ..........................................................................................
III. Pregnancy ..........................................................................................

Date .......................................... Signature ..........................................

Station .......................................... Desogmatopm ..........................................

# FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI YA KUKUBALI SHERIA ZA SHULE.

## 1. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI.

- Jina kamili la mwanafunzi ..........................................................................
- Tarehe ya kuzaliwa ..........................................................................
- Mnaishi/Mnakaa wapi? (Kata na Kijiji/Mtaa) ..........................................................................
- Uraia: MTANZANIA/SIO MTANZANIA: ..........................................................................
- Shule aliyotoka ..........................................................................
- Namba ya mtihani (PS) ..........................................................................

..........................................................................

## 2. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI:

- Jina la Mzazi/Mlezi ..........................................................................
- Kazi ya Mzazi/Mlezi..........................................................................
- Anwani ya Mzazi/Mlezi..........................................................................
- Simu ya Mzazi/Mlezi..........................................................................
  (Kama huna nambari ya simu ya jirani yako)..........................................................................
- Ndugu/Jamaa wa karibu wa mwanafuni.

| Na. | Jina la Jamaa/Ndugu | Namba ya simu | Anapoishi | Uhusiano |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |

## 3. AHADI YA MWANAFUNZI:

**Mimi** ..........................................................................**nimesoma na kuyaelewa** maelekezo yote ya kujiunga na shule ya sekondari ..........................................................................na Nimekubali/Sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Ninaahidi kufuata na kutekeleza sheria na taratibu zote za shule, kusoma kwa bidii na niko tayari kupokea adhabu yoyote endapo nitavunja utaratibu wa shule kwa makusudi.

**Sahihi:** .......................................................... **Tarehe:** ........................................

## 4. AHADI YA MZAZI/MLEZI:

Mimi ..........................................................................Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi Ninaahidi/siahidi kushirikiana kwa karibu na uongozi wa shule katika malezi ya mwanangu. Pia nitampatia mwanangu mahitaji yote muhimu (fedha na vifaa) kama uongozi wa shule ulivyoelekeza. Vile vile niko/siko tayari kuupokea uamuzi utakaotolewa na uongozi wa shule endapo mwanangu atavunja sheria na taratibu za shule ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo, kupewa adhabu au kufukuzwa shule.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi .......................................................... Tarehe: